OFISI YA RAIS - TAMISEMI

HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI

SHULE YA SEKONDARI ya ufundi MOSHI.

S.L.P 3014 Moshi, Simu 0755 011 478, Barua pepe: moshitechnical63@gmail.com

Ndugu……..

…….

……

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO 2022/2023

Tunafurahi kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga na shule hii kwa masomo/mchepuo wa…… Shule hii ni ya bweni na ni ya mchanganyiko kwa Kidato cha I hadi cha 4 (Wavulana na wasichana). Iko umbali wa kilometa tano kutoka kituo cha mabasi Moshi Mjini, Kando ya barabara Kuu ya Moshi – Arusha. Wewe ni miongoni mwa wanafunzi wachache waliobahatika kuchaguliwa kuendelea na masomo katika shule hii ya sekondari ya Moshi Ufundi. Kuchaguliwa kwako ni deni kubwa kwa Nchi yako, Serikali na wananchi. Ukija hapa ni kama umetumwa na Wananchi wa Tanzania uje uvune chochote na urudi kuwasaidia ukishavuna, "HILI LIWE NDILO LENGO LAKO KUU UTAKAPOKUWA HAPA SHULENI".

Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **.....** Nafasi yako itachukuliwa na mwanafunzi mwingine kama utashindwa kuripoti ndani ya wiki 2 baada ya tarehe ya kufungua. Ifahamike kuwa Elimu bila malipo ni kwa kidato cha kwanza hadi cha nne. Kidato cha Tano na Sita wanalipa ada na michango ya shule. Mzazi/Mlezi unasisitizwa kumlipia mwanao au uwasiliane na Mamlaka husika itakayomlipia mwanao ili aweze kupokelewa shuleni. Inasisitizwa ulipe malipo hayo mwanzoni mwa muhula. Malipo yafanyike kupitia Akaunti ya shule Na.**40301200138** NMB. Jina LA Akaunti ni **MOSHI TECHNICAL SECONDARY SCHOOL**.

Hakikisha una nauli ya kurudi nyumbani kila shule inapofungwa. Aidha, jaza fomu zilizoambatanishwa na ziwasilishwe shuleni wakati wa kuripoti.

E.S. KYARA
MKUU WA SHULE

MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE MWAKA 2020/2021

KAULI MBIU YA SHULE NI:

- Kutii
- Kuwajibika
- Kubuni

Kauli mbiu hiyo ndiyo dira yako utakapokuwa hapa shuleni kwa kipindi chote cha miaka 2. Unatakiwa uitafakari na kuifanyia kazi kwa vitendo. Ni matumaini yetu kuwa utatumia nafasi hii adimu kwa manufaa yako, jamii yako na Taifa kwa ujumla.

A. **ADA NA MICHANGO.**

1. Ada ya shule…..……..Tsh.70,000/= (kwa Mwaka)
   Tahadhari (fedha hii hairudishwi) Tsh. 5,000/=
   Kitambulisho na picha…… Tsh.6,000/=
   Mchango wa Taaluma…….Tsh.20,000/= (kwa Mwaka)
   Samani na ukarabati …… Tsh.15,000/=
   Matibabu …….Tsh. 15,000/=(kwa Mwaka)
   Ulinzi , wapishi na vibarua wengine …….Tshs.30,000/=(kwa Mwaka)
   Nembo ya shule……Tsh...2,000/=

   JUMLA Tsh.163,000/=

NB. Baadhi ya wanafunzi sio waaminifu na hutumia ada na michango ya shule kwa mambo yao binafsi. Mzazi/mlezi hakikisha unalipa ada na michango yote benki na mwanafunzi aje na Bank-Pay-Slip tu yenye jina la mwanafunzi, na iwe halisi na sio kivuli (photocopy). Hakikisha pia umetoa nakala mbili (photocopy ya Bank-Pay-Slip)

B. **Sare ya shule**

- Suruali mbili za rangi ya Ugoro (Tobacco)
- Shati mbili nyeupe mikono mifupi
- Sweta 1 ‘la rangi ya ugoro (Tobacco)
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba visiwe na visigino virefu.Soksi nyeupe jozi mbili.
- Mkanda mweusi wa ngozi (usiwe na bakoli kubwa sana)
- Nguo za michezo (i) Bukta na T-shirt rangi ya bluu bahari (ii) Raba nyeusi za michezo.
- Traki suti rangi ya **Dark Blue** kwa ajili ya kujikinga na baridi wakati wa kujisomea usiku (Preparation).
- Koti jeupe la mikono mirefu la maabara. (LAB COAT)
- Picha 2 za passport alizopiga akiwa amevaa shati jeupe
- Nguo za kushindia: suruwali nyeusi na T- shirt nyekundu au kijani isiyokua na maandishi.

C. **MAHITAJI BINAFSI**

- Godoro la sponji futi 2½, mto na foronya 2 za bluu bahari
- Blanketi 1, shuka 2 za rangi ya bluu bahari
- Chandarua kwa ajili ya kujikinga na mbu
- Vifaa vya kulia chakula (sahani, bakuli, kikombe na kijiko)
- Ndoo ya kuogea MBILI
- Madaftari makubwa (Counter book) zisizopungua 10
- Begi la kubebea madaftari na liwe la kuvaa mgongoni
- Taulo na ndala za kuogea
- Sandles za rangi nyeusi kwa ajili ya kushindia nje ya darasa.
- Sabuni, kiwi na brush ya viatu
- Baadhi ya vitabu vya masomo (angalia orodha iliyoambatanishwa)
- 'Dissection kit' kwa mwanafunzi anayesoma Biolijia (PCB na CBG).
- Scientific calculator
- Faili la kutunzia mitihani yake ya ndani (mitihani inayofanyika shuleni)

D. **VIFAA VYA USAFI SHULENI.**

Kila mwanafunzi kutegemeana na 'combination' yake atatakiwa kuleta vifaa vifuatavyo kwa ajili ya kufanyia usafi awapo shuleni.

- **PCM** -walete Fekeo, Soft broom1, hard broom 1,dawa ya chooni lita 5, squizer 1 na chelewa yenye mpini
  (Street broom)
- **PCB –** Walete, Reki 1, Soft broom 1, hard broom 1, dawa ya chooni lita 5, Squizer 1, na chelewa yenye mpini (Street broom) 1.
- **CBG –** Walete Jembe 1, Soft broom 1, brashi ya kusafishia choo (Toilet sink brush complete) 1, dawa ya chooni lita 5, squizer 1, na chelewa yenye mpini (Street broom) 1.

N.B Baadhi ya vifaa kama vile vifaa vya usafi , madaftari, Scientific calculator, RIM PAPER na LAB COAT Vinapatikana kwenye maduka yaliyo jirani na shule.

*Vifaa vyote vilivyoagizwa vitakaguliwa katika ofisi ya usajili kabla ya mwanafunzi kusajiliwa

MAAGIZO MENGINE

1. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na bima ya afya. Mzazi hakikisha mwanao ana bima ya afya anaporipoti shuleni.
   - Wagonjwa wanatakiwa kufika katika zahanati ya shule saa 1.30 asubuhi kwa matibabu
   - Itokeapo dharura ya ugonjwa wakati wa masomo itamlazimu mwanafunzi kupata kibali cha maandishi kutoka kwa mwalimu ili aweze kutibiwa.
   - Ili kutibiwa katika Hospitali ya Wilaya au ya Mkoa ni lazima mwanafunzi aruhusiwe na Mhudumu wa zahanati ya shule.
   - Iwapo mwanafunzi atalazwa hospitali kwa ugonjwa ni sharti arudi shuleni mara tu anaporuhusiwa kutoka hospitalini na kutoa taarifa kwa Mkuu wa shule.
2. Wanafunzi wote wanatakiwa kuja na **RIM PAPER MBILI** nyeupe wanaporipoti shule.

A. SIKU YA WAGENI

Wanafunzi wanaweza kutembelewa na ndugu au jamaa zao mara moja kwa mwezi na siku hiyo ni Jumapili ya kwanza ya mwezi kuanzia saa 8 hadi saa 10 jioni.(mzazi unapomtembelea mtoto haruhusiwi kuja na chakula wala vinywaji)

NYARAKA MUHIMU ZA KUJA NAZO SHULENI.

Mwanafunzi anatakiwa akamilishe/ajaze fomu zifuatazo.

(i) Fomu ya kukubali nafasi/Sheria za shule ikiwa imesainiwa na Mzazi/Mlezi baada ya kuzisoma zote kwa pamoja na kuzielewa.

(ii) Fomu ya taarifa binafsi pamoja na orodha ya ndugu na jamaa wa mwanafunzi (Ijazwe na Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi).

(iii) Ahadi ya mzazi/mlezi atakayemlipia mwanafunzi ada na michango yote ya shule.

(iv) Nakala ya cheti cha kuzaliwa.

(v) Fomu ya kupimwa afya (Medical Examination).

(vi) Nakala ya matokeo ya kidato cha nne (Result Slip) (leta photocopy)

NB. Ni lazima Mwanafunzi aje na**"Joining Instruction"** hii ikiwa imejazwa kikamilifu na pia mwanafunzi hatapokelewa bila nakala ya matokeo ya kidato cha nne (result slip) kwa kua ndio kitambulisho cha mwanafunzi.

TAHADHARI: "Tunza fedha na vifaa vyako uwapo safarini. Epuka kupokea vyakula kutoka kwa mtu usiyemfahamu.

Nakutakia Safari njema na
KARIBU SANA SHULENI MOSHI UFUNDI.

E.S. KYARA
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI UFUNDI MOSHI
S. L.P. 3014 — MOSHI

Nakala: Katibu Mkuu,
OR - TAMISEMI,
S.L.P. 1923, **DODOMA.**

: Katibu Mkuu,
Wizara ya Elimu,
DODOMA.

: Mkurugenzi,
Manispaa ya Moshi,
S.L.P. 318, **MOSHI.**

: Mdhibiti Mkuu ubora wa Elimu,
Kanda ya Kaskazini Mashariki,
S.L.P. 460,**MOSHI**.

: Maafisa Elimu wa Mikoa.

FOMU YA KUKUBALI NAFASI NA SHERIA ZA SHULE

I. **Mwanafunzi**

Jina Mwanafunzi……

Anuani……

Mimi……nimekubali kujiunga na Jumuiya ya Shule ya Sekondari ya Moshi Ufundi. Nimesoma maagizo ya Shule kwa makini na kuyaelewa. Naahidi kuwa mtiifu na nitazingatia sheria, na taratibu zote za shule kama nitakavyoelezwa.

Saini ya Mwanafunzi……Tarehe……

II. **MZAZI/MLEZI.**

Mimi ……Mzazi/Mlezi wa……

Nimesoma kwa makini maagizo ya shule yaliyotolewa kwa mtoto wangu. Nimekubali mwanangu achukue nafasi hiyo. Naahidi kuwa nitashirikiana na Uongozi wa shule katika kumkuza na kumlea mwanafunzi huyu kielimu na Kitabia.

Saini ya Mzazi/Mlezi…….Tarehe…….

ZINGATIA/SISITIZO

- Hakikisha Mwanao haji nasimu Shuleni. Akipatikana nayo adhabu kali itatolewa ikiwa ni pamoja na kurudishwa nyumbani. Hili ni agizo la Serikali.

- Mzazi/Mlezi hakikisha mwanao amezisoma Sheriazote za Shule zilizoambatanishwa na mzitafakari ndipo usaini fomu hii.

SHERIA ZA SHULE

Mwanafunzi anatakiwa:-

1. Kuwaheshimu waalimu, wafanyakazi wengine wote na wanafunzi wenzake.
2. Kusimama na kumsalimu mtu yeyote anayemzidi umri mara tu anapokutana naye nje au ndani ya shule.
3. Kushiriki katika kazi zote atakazopangiwa darasani na nje ya darasa ikiwa ni pamoja na usafi wa shule kwa ujumla. Mwanafunzi asiyekuwa na utayari wa dhati wa kushiriki shughuli za usafi wa shule anashauriwa kutafuta shule nyingine.
4. Kuhudhuria masomo/vipindi wakati wote na kufanya mitihani. Kama kuna sababu ya kutokuhudhuria au kufanya mitihani ielezwe kwa Mkuu wa shule mapema.
5. Kuwahi shuleni wakati shule inapofunguliwa baada ya likizo.
6. Kuvaa sare ya shule anapokwenda na kurudi likizo.
7. Kuzingatia na kutunza/kufuata ratiba ya shule
8. Kuwa msafi na kutunza mazingira.

Vilevile mwanafunzi hatakiwi/haruhusiwi:

1. Kuvuta sigara, bangi wala madawa ya kulevya.
2. Kufuga kucha, nywele wala ndevu.
3. Kuvaa mavazi yasiyo na heshima kama milegezo na suruwali za kubana.
4. Kupigana au kugombana.
5. Kunyoa nywele mitindo ya kihuni kama kipara/panki.
6. Kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa ya mwalimu.
7. Kutumia lugha chafu.
8. Kwenda nyumba za waalimu na watumishi wengine bila kibali.
9. Kuingia na mgeni yeyote bwenini au madarasani
10. Kutembelea vilabu vya pombe au majumba ya kufikia wageni
11. Kuharibu mali ya umma kama madawati, viti, vitanda, vyoo, madirisha, vitabu, vifaa vya maabara n.k. Akifanya hivyo atalipishwa.
12. Kuwa na jiko, heater, redio na vifaa vingine vyovyote vinavyotumia umeme.

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE KABISA.

1. Wizi
2. Uasherati
3. Ulevi wa aina yoyote
4. Ubakaji
5. Ushoga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuoa
9. Kumpa mimba msichana/mwanamke
10. Makosa ya jinai
11. Kutohudhuria vipindi vya masomo mfululizo kwa miezi miwili bila sababu ya msingi.
12. Kukataa adhabu halali kwa makusudi
13. Kumiliki simu, redio, Camera, Ipad au kifaa chochote kinachoelekeana na hivyo.
14. Kuanzisha, kuchochea na kushiriki mgomo au kufanya maandamano yasiyo halali.
15. Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake , mtumishi au mwalimu.

N.B mwanafunzi hatakiwi kuja na simu shuleni anapokuja kuripoti na shule haitahifadhi simu ya mwanafunzi yeyote. (mawasiliano yote yanafanyika kupitia simu ya shule 0755011478)

ORODHA YA VITABU KWA KILA SOMO

Tunashauri mzazi /mlezi mwenye uwezo (siyo lazima) amnunulie mwanae vitabu vifuatavyo kuendana na mchepuo wake na 'Reviews ' za masomo mbalimbali.

1. **PHYSICS**
   (i) A level Physics by Roger Muncaster (4th Edition)
   (ii) A level Physics by Nelkon and Parker (7th Edition)
   (iii) A Level Physics by Tom Duncan (3rdEdition)

2. **CHEMISTRY**
   (i) Organic Chemistry Volume I
   (ii) Advanced level Inorganic chemistry Part I & II (TIE 1995)
   (iii) Advanced Chemistry review by William W. Davis (Mzumbe Book Project 2004)
   (iv) Physical Chemistry by Delungu (Mzumbe Book Project, 1998)

3. **MATHEMATICS**
   (i) Advanced Mathematics volume I and II (Ministry of Education and Vocational Training)
   (ii) Pure mathematics Vol. I & II by Back House
   (iii) Advanced Mathematics By Tranter and Laube
   (iv) The core course for A level by Bastock and Chandler
   (v) Advanced Mathematics by Shayo.

4. **GEOGRAPHY**
   (i) Integrated Approach to physical Geography (Msabila)
   (ii) Integrated Geography (By F. J. Monkhouse))
   (iii) Map reading for East Africa
   (iv) Principles of Geography (By F.J. Monk house)
   (v) General Geography in diagram(By R.P. Bunget)
   (vi) Simplified Physical Geography for a level (By D.M.Mapunda)

5. **GENERAL STUDIES**
   (i) Any General Studies Book for 'A' Level.

6. BIOLOGY

(I) Biological Science

TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

SEHEMU A:

1. Jina (MAJINA MATATU)……
2. Tarehe ya kuzaliwa……
3. Uraia…….Mkoa……Wilaya……
   ……...Kabila……..
4. **Taarifa ya kubaini wanafunzi Yatima**

   Weka alama ya vema (√) panapohusika.

   (i) Baba na Mama wote walikwishafariki( )

   (ii) Baba yupo, Mama alikwishafariki ( )

   (iii) Mama yupo Baba alikwishafariki ( )
5. Jina la Baba/Mlezi……Kazi yake……

   Anwani ya Baba/Mlezi……

   Namba ya simu ya Baba/Mlezi……

   Anwani ya anakofanyia kazi……
6. Jina la Mama/Mlezi…….Kazi yake…….Anwani ya Mama/Mlezi……

   Namba ya simu ya Mama/Mlezi……
7. Je, wazazi wako huishi pamoja? Ndiyo/Hapana……
8. Je, unaishi na wazazi wako wakati wa likizo? Ndiyo/Hapana. Kama huishi nao eleza unaishi na nani?
9. Jina……..Anwani yake……Una uhusiano gani naye……
10. Dini unayofuata……Dhehebu…… (waje na vitabu vya dini zao)
11. Taarifa za maendeleo zitumwe kwa nani?
    Jina……Anwani yake……

12.je wazazi wote wapo hai? Ndiyo/hapana …….je una mzazi mmoja ? taja (baba/mama)……je huna wazazi kabisa ndiyo / hapana ……

TAARIFA KUHUSU SHULE ULIYOTOKA:

(i) Jina la Shule……

(ii) Anwani ya Shule hiyo …….

(iii) Namba uliyofanyia mtihani……

ORODHA YA NDUGU/JAMAA WA MWANAFUNZI:

Fomu hii ijazwe na kila mwanafunzi akitoa maelezo sahihi ya Ndugu, Jamaa zake watano watakaompa huduma mbalimbali wakati akiwa hapa shuleni. Watakaoorodheshwa hapa ndio pekee watapata ridhaa ya kushughulikia masuala ya mwanafunzi awapo shuleni hususani yanapotokea matatizo ya kinidhamu.

S/N	JINA LA NDUGU/JAMAA	MNAVYOHUSIANA	ANWANI YAKE NA NAMBA YAKE YA SIMU
1			
2			
3			
4			
5			

NATHIBITISHA KUWA TAARIFA HII NI SAHIHI:

Sahihi ya Mzazi/Mlezi……

Tarehe……

MOSHI TECHNICAL SECONDARY SCHOOL MEDICAL EXAMINATION FORM.

To be completed by a Medical Officer (Government hospital)

NAME:……..FORM……

BLOOD COUNT

(Red and White) ……

STOOL EXAMINATION……

URINE ANALYSIS ……..

STAPHILIA TEST……..

T.B. TEST…….

EYE TEST……..

EARS……..

CHEST……...

SPLEEN……

ABDOMEN……..

ADDITIONAL information e.g. Physical defects or impairments……

……

Infections; chronic or family diseases etc

……

Please certify that the above is fit to be enrolled at Moshi Technical Secondary School

Signature……. Designation…….

Station…… Date……..

NB.TO MEDICAL OFFICER: At the time of examination please TREAT the individual for any

Ailment you note.